

UNITED NATIONS



NATIONS UNIES

THE SECRETARY-GENERAL

--

VIDEO MESSAGE TO MODEL UNITED NATIONS

December 2023

Asanteni kwa kushiriki katika muundo wa Baraza Kivuli la Umoja wa Mataifa na kuwa waumini katika nguvu ya ushirikiano wa kimataifa katika kutatua matatizo yanayoikabili dunia.

Dunia yetu inahitaji ushiriki wako pamoja na mawazo yako kuliko ilivyowahi kuhitajii hapo awali.

Tunaishi katika nyakati ngumu sana

Mizozo inachachamaa, hali ya uhasama inaongezeka, na sayari yetu inaungua

Mahitaji ya kibinadamu yanahitajika kwa kiwango kikubwa zaidi na haki za binaadamu zinakiukwa kiholela

Matamshi ya chuki, taarifa zenye upotoshaji na kutokutoa taarifa sahihi kwa makusudi kunaenea kwa kasi kaika mitandao ya kijamii.

Zaidi ya hapo awali, tunahitaji mshikamano wa kidunia.

Tunaihitaji Umoja wa Mataifa.

Na Umoja wa Mataifa unakuhitaji wewe-nguvu zako, ubunifu, ujasiri, na kujitolea kwako.

Kwa pamoja, ninajua tuna kile kinachohitajika kutatua changamoto zetu.

Kuponya utangano, kurekebisha mahusiano, na kujenga amani.

Kutoa mkono wa msaada kwa wale wote waliogubikwa na vita, janga la Mabadiliko ya Tabianchi na Njaa.

Kuhakikisha Haki na usawa kwa wanawake na wasichana duniani na kwa jamii zilizo pembezoni hasa walio na hali duni duniani.

Na kueneza fursa kwa wote, bila kumuaha mtu yeyote nyuma.

Sisi tuliopo katika Umoja wa Mataifa hatuta kata tamaa katika kusaka dunia yenye amani na haki.

Na ninafahamu kwamba hata wewe pia hautakata tamaa.

Ndiyo maana ninajitolea vilivyo katika kuwapa vijana sauti imara zaidi kwenye masuala ya kimataifa.

Umoja wa Mataifa unafurahia kuwa rafiki yako. Na tunakutegemea kuwa na jitihada zenye kuleta mabadiliko chanya saa na katika siku za usoni. Nakutakia kila la heri.

Asante

\*\*\*